**30 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 30 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kigua.

Na. 455

**Kuzipandisha Hadhi Shule za Sekondari Seuta, Kimbe na Kikunde – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Shule za Sekondari Seuta, Kimbe na Kikunde - Kilindi kuwa za kidato cha tano na sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari Seuta, Kimbe na Kikunde ni shule zilizopo kwenye mpango wa kupandishwa hadhi kuwa za kidato cha tano na sita. Shule ya Sekondari Kikunde tayari imepata kibali kupitia barua yenye Kumbukumbu Na. ED.280/315/5055/9 cha tarehe 03/07/2024 na itaanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano Julai, 2025. Aidha, Shule za Sekondari Seuta na Kimbe bado hazijakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2025 Shule ya Sekondari Kimbe imepokea shilingi milioni 130 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kidato cha tano. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika Shule za Sekondari Seuta, Kimbe na Kikunde kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali na Wana-Kilindi wanashukuru sana kwa kupokea shilingi milioni 130 kwa ajili ya bweni pale Kimbe Sekondari, lakini halikadhalika kwa ajili ya Shule ya Sekondari Kikunde kupokea wanafunzi mwezi Julai.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba sasa ni lini Serikali itatoa shilingi milioni 30 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Seuta ili kukamilisha bweni la wavulana na ili kupokea wanafunzi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Omari Kigua kwa kweli amekua akifanya ufuatiliaji mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba sekta hii muhimu kabisa ya elimu msingi katika jimbo lake inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpa taarifa kwamba hata katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita, kipindi cha miaka minne tayari Serikali imekuwa ikijenga miundombinu muhimu kabisa ya kuwawezesha wanafunzi wetu kusoma, lakini ikiwemo kuendelea kujenga miundombinu katika shule za kidato cha kwanza mpaka cha nne ili ziweze kupata miundombinu inayohitajika kupata usajili wa kuwa kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie kwamba Serikali inatambua; na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge tumezungumza mahsusi kabisa kuhusiana na hii shilingi milioni 30 ambayo itatengwa kwenye mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kujenga bweni katika shule hii ya Seuta ili wanafunzi hawa katika shule hii wapate bweni la wavulana na weweze kusoma, wapate sehemu nzuri ya kupatia masomo yao.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali italifanya hilo, itatenga hii fedha, itaileta kwa ajili ya kujenga bweni hili katika shule hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 456

**Ujenzi wa Shule za *A - Level* Nchini**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu kujenga shule za sekondari za *A - level* kama ilivyofanya kwa shule za msingi na sekondari ili kukabiliana na wingi wa wanafunzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikijenga shule mpya za kidato cha tano na kujenga miundombinu katika shule za sekondari zilizopo ili kuzipandisha hadhi kuwa na wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020 hadi 2024 kumekuwa na ongezeko la shule 254 za kidato cha tano na sita kutoka shule 401 hadi shule 655. Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi 109,540 (wavulana 62,206 na wasichana 47,334) hadi wanafunzi 207,696 (wavulana 104,830 na wasichana 102,866).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kujenga shule mpya za kidato cha tano na sita na kupandisha hadhi shule zilizopo kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa ongezeko hilo la shule hizo za A-*Level,* lakini bado tumejenga shule nyingi sana za hapa chini, kwa hiyo tunakuwa na wanafunzi wengi mno wakielekea kwenda kidato cha tano na cha sita.

Je, hamuoni umuhimu sasa katika kila shule inayojengwa lazima yawepo mabweni kwa ajili ya kuwahifadhi wanafunzi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri ninatambua kabisa kwamba katika shule nyingi ambazo mmejenga kuna baadhi ya shule zina wanafunzi wengi bado wako *A – Level,* kwa mfano, Shule ya Sekondari ya Kibisi iliyopo katika Wilaya ya Rungwe ina wanafunzi wengi sana lakini haina *A-Level;* je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuweza kuwawezesha kuweza kujenga madarasa mapya ya *A- Level?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwa swali lake hili zuri kabisa linalolenga kuzungumzia uimarishaji wa sekta muhimu hii ya elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza ni dhahiri kabisa katika utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo udahili wa wanafunzi umeongezeka maradufu na mahitaji ya miundombinu ya shule zetu yameongezeka. Serikali kwa upande huo imefanya uwekezaji mkubwa sana kuendana na uhitaji. Zaidi ya shilingi trilioni 5.1 zimewekezwa katika sekta hii muhimu ya elimu msingi na sekondari kwa ajili ya kujenga shule, kwa ajili ya kujenga madarasa, lakini kuboresha miundombinu yote muhimu kwa ajili ya kuwezesha wanafunzi wetu kupata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, shule mpya 1,349 zimejengwa zikiwemo shule za sekondari za kata 694 lakini kuna shule mahsusi za

wasichana 26 za bweni za sayansi zimejengwa kila mkoa shule moja, lakini kuna shule 103 za Amali. Kwa hiyo, utaiona dhamira ya Sekrikali ya Awamu ya Sita kuendelea kuboresha katika upande wa miundombinu kwa ajili ya watoto wetu kupata shule za kusomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mabweni; katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita zaidi ya mabweni 2,308 yamejengwa na mabweni haya yanawezesha watoto katika shule zile ambazo zina miundombinu kwa ajili ya kidato cha kwanza mpaka cha nne ziweze kupandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na sita ili kuendelea kuongeza shule hizi ambazo zinapokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita wanafunzi wetu waweze kupata sehemu ya kusomea. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uhitaji wa madarasa katika shule uliyoitaja katika Wilaya ya Rungwe, ninaomba nikuhakikishie kwamba Serikali itaendelea kuboresha miundombinu katika sekta hii muhimu kabisa ya elimu msingi na sekondari na hata katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita zaidi ya madarasa 60,000 yamejengwa kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu hii ya shule zetu ili wanafunzi wale wengi ambao wamejitokeza kupata udahili na kusoma katika shule hizi waweze kupata maeneo mazuri ya kupatia elimu yao.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Serikali ya Awamu ya Sita ipo kazini na itaendelea kuimarisha sekta hii muhimu kabisa ya elimu msingi na sekondari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mama Malecela umesimama? Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Shule za Funvuhu, Kidia na Matemboni Kata ya *Old Moshi* Mashariki Shule zile zimechakaa kabisa na zinavuja ni za muda mrefu. Ni lini Serikali itakwenda kurekebisha majengo haya ili watoto waweze kusoma vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Felista Njau kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kuimarisha sekta hii muhimu kabisa ya elimu msingi na sekondari na ndiyo maana utaona uwekezaji mkubwa sana umefanyika, zaidi ya shilingi trilioni 5.1 zimetoka katika kipindi cha miaka minne tu kwa ajili ya kuboresha sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la miundombinu ni sehemu mahususi kabisa ambalo Serikali inaweka msukumo kwa kuendelea kujenga shule mpya, lakini kukarabati shule zile ambazo zimechakaa. Hata katika kata hii ya *Old Moshi* Mashariki katika shule ulizozitaja Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri lakini kwa Serikali Kuu kuunga mkono na kuongeza nguvu itafika kwa ajili ya kuzikarabati shule hizi ili ziweze kuwanufaisha wananchi, na kwa kweli hata Mheshimiwa Profesa Ndakidemi amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu kabisa katika kuhakikisha hili linafanikiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Mariam Nyoka.

Na. 457

**Ujenzi wa Barabara ya Kiuma hadi Kalulu**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Barabara ya Kiuma hadi Kalulu Songea kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa Barabara ya Milonde - Kalulu ambayo kukamilika kwake kutachochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Tunduru. Barabara hii ina urefu wa kilometa 26.8 na inaunganisha barabara kuu katika Kijiji cha Milonde kwenda Kata ya Kalulu kuelekea Mbuga ya Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024/2025 barabara hii inafanyiwa matengenezo kwa shilingi milioni 362.29 ambazo ni fedha za maendeleo ya jimbo na hadi sasa barabara hii inaendelea kujengwa ambapo kazi zinazofanyika ni pamoja na uchongaji wa barabara kilometa 26.8, uwekaji wa kifusi cha changarawe kilometa 19, ujenzi wa kalavati mbili *(pipe culvert),* pamoja na ujenzi wa kingo za Daraja la Mto Muhuwesi zilizoathiriwa na mvua za mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuihudumia na kuiboresha Barabara ya Milonde - Kalulu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ya kutoka Mtina kuelekea Nasya hadi Namasakata kwa kiwango cha changarawe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lingine, lini Serikali itatengeneza barabara ya kutoka Nalasi Mashariki kuelekea Chinganga hadi Nasomba kwa kiwango hicho cha changarawe? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mariam Nyoka kwa hakika amekuwa akifanya ufuatiliaji wa hali ya juu katika upande huu wa kuimarisha miundombinu ya upande wa barabara na hasa hizi za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mariam kwamba katika kipindi cha miaka mitano katika Wilaya hii ya Tunduru tayari shilingi bilioni 13.9 zimetumika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi zinazohudumiwa na *TARURA*. Pia katika mwaka wa bajeti 2025/2026 fedha imetengwa kwa ajili ya kuendelea kuhudumia miundombinu hii ya barabara.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itahakikisha inafikia barabara hii ya Mtina – Nasya - Namasakata na pamoja na barabara hii ya Nalasi Mashariki Chinganga – Nasomba kwa ajili ya kuzipandisha hadhi kuwa katika hadhi ya barabara za changarawe ili kwa hatua hii ziweze kuanza kutoa huduma bora zaidi kwa ajili ya wananchi kufikia huduma za kijamii, lakini pia kufanya shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, je, Barabara ya Ilula – Uhambingeto inayokwenda Ilambilelo inakuja kutokeza mpaka barabara inayounganisha na Dodoma. Ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami au tu kuboreshwa ili magari yasiendelee kupita kule mjini yaweze kupita tu hapa kwenye hii barabara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa swali lake hili zuri kabisa. Ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi za Wilaya zinazohudumiwa na *TARURA* na dhamira hiyo ya dhati utaiona hata katika ongezeko la bajeti ya *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni shilingi bilioni 275 kwa mwaka, lakini tangu Serikali ya Awamu ya Sita imeingia madarakani imeongeza bajeti hiyo maradufu na mpaka wakati huu tunatarajia katika mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya *TARURA* itakuwa ni shilingi trilioni 1.18. Kwa hiyo, unaona kabisa dhamira ya dhati ya kuendelea kuwekeza katika upande huu wa barabara hizi za *TARURA* ambazo zinawasaidia sana wananchi kufikia huduma za kijamii, lakini kufanya mambo yao ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusiana na Barabara hii ya Ilula katika Jimbo la Kilolo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, ninaomba nikuhakikishie kwamba Serikali itafika na italeta fedha kwa ajili ya kupandisha hadhi, kukarabati na kuweka katika hali nzuri barabara hii ili iweze kupitika katika kipindi cha mwaka mzima ili wananchi waweze kufanya shughuli zao za uzalishaji mali, lakini pia waweze kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Cherehani.

Na. 458

**Maeneo ya Malisho ya Mifugo – Ushetu**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga eneo la malisho wafugaji katika Halmashauri ya Ushetu ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza shughuli za kuainisha na kutenga maeneo ya malisho ya mifugo ili kuboresha shughuli za ufugaji na kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Ushetu inaendelea na utaratibu za kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya wafugaji ambapo jumla ya hekta 179,593 zinatumika kwa shughuli za ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutenga maeneo hayo, Serikali imeendelea kuboresha malisho, ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 halmashauri imetenga kiasi cha shilingi millioni tano kwa ajili upatikanaji wa malisho na ununuzi wa mbegu. Aidha, Halmashauri ya Ushetu imetoa elimu kwa vikundi 23 vya wafugaji katika kata 20 zenye maeneo yanayoweza kulimwa malisho ya mifugo yenye jumla ya ekari 477. Aidha, halmashauri imetenga shamba darasa la malisho katika Kata ya Ushetu, Kijiji cha Ibelansuha lenye ukubwa ekari saba ambalo limepandwa malisho aina ya *rhodes* na *blue pea* kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia wafugaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, niendelee kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri kwa wananchi wetu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya ekari hizo 175,593 ni yale maeneo ambayo yanaingiliana na wananchi ambao

wanayasimamia wao kitu ambacho bado inaongeza migogoro ya wafugaji na wakulima wetu. Halmashauri ya Ushetu ina mapori ya *Usumbwa Forest Reserve,* tuna Mpunze Saba Sabini na tuna *Ubagwe Forest Reserve*. Ni mapori ya halmashauri, Baraza la Madiwani limekaa, zaidi ya miaka minne tunaendelea kuomba angalau mojawapo tuweze kutengewa kwa ajili ya wafugaji ili kutoingiliana na haya maeneo ambayo yapo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lini Serikali itatuma timu yake ije angalau iyabaini mapori haya ili sasa kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji inayoendelea katika Halmashauri ya Ushetu? Ili wakulima hawa tuwatengee eneo la malisho angalau wawe wanachangia hata kiasi kidogo kwa kila kichwa cha mfugo mmoja wa ng'ombe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa mujibu wa taratibu, sheria na miongozo mbalimbali ya matumizi ya ardhi Mamlaka za Serikali za Mitaa ndizo zenye wajibu wa kupanga matumizi bora ya ardhi kwa kuainisha maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo, shughuli za kilimo na kwa ajili ya uhifadhi kulingana na mazingira katika halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge dhamira ya Serikali ni kuendelea kuhakikisha tunatenga maeneo kwa ajili ya mifugo na maeneo kwa ajili ya wakulima ili kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Ushetu kwa kutambua misitu hiyo ambayo mapendekezo ya baraza ni kuwa maeneo ya malisho ili kuondoa migogoro kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali iko tayari itatuma wataalam wafike Ushetu

muweze kuwapitisha katika maeneo hayo ili waweze kutoa ushauri wa kitaalamu na kukubaliana na baraza namna nzuri ya kutumia maeneo hayo ili kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Sitta.

Na. 459

**Ujenzi wa Gereza Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya Gereza la Urambo kwa kuwa lililopo limechakaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza Urambo ni miongoni mwa magereza yaliyojengwa mwaka 1981 likiwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 150 kwa siku. Katika kukabiliana na uchakavu wa miundombinu ya Gereza la Urambo na nagereza mengine, Serikali kupita Jeshi la Magereza imeanza kutekeleza mpango mkakati wa ukarabati wa miundombinu chakavu ya Magereza kwa awamu. Sambamba na kujenga magereza mapya kwenye Wilaya zisizokuwa na magereza nchini. Gereza la Urambo litaingizwa kwenye mpango wa awamu ya pili ya Mpango wa Ukarabati wa Magereza kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Sitta.

**MHE. MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali ambayo yanatupa matumaini kwa siku zijazo. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; hali ya mahabusu pale Urambo ni ya hatari sana. Kwanza, kutokana na miundombinu chakavu ya maji machafu, halafu pili, chumba wanacholala hakijakamilika tangu mwaka 2013.

Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kuhusu hali hiyo ambayo ni hatarishi? *(Makofi)*

Swali la pili, mpaka sasa mahabusu hiyo haijawa na gari hata siku moja. Je, Serikali inasemaje kuhusu kuwapa gari ili liwasaidie katika shughuli zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa hatua ya dharura niwaelekeze wataalam wetu wa Jeshi la Magereza kwenda Urambo kufanya tathmini ya haraka na kuona namna bora ya kuboresha eneo hilo ili kuokoa majanga kwa wafungwa na mahabusu walioko gereza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu gari, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Gereza la Urambo litakuwa kwenye mpango ili magari yanayokuja basi mojawapo liende Urambo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wafungwa na mahabusu wa Gereza la Urambo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe kwa niaba Mheshimiwa Raymond.

Na. 460

**Hitaji la Nyumba za Polisi - Hai**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga nyumba za askari polisi katika Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Hai?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Wilaya ya Hai ina eneo la kambi ya kuishi askari polisi lenye ukubwa wa mita za mraba 8,092 na eneo liko katika Mtaa wa St. Dorcus. Kwa sasa eneo hilo lina nyumba nane za makazi zinazoishi familia 16 za askari. Serikali ina mpango wa kuendelea kujenga nyumba za makazi ya askari eneo hilo na kwa kuanzia inatarajiwa kujenga nyumba moja ya ghorofa itakayoweza kuishi familia nane za askari na kwenye eneo la Kituo cha Polisi cha Wilaya kunatarajiwa kujengwa nyumba ya Mkuu wa kituo. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Uhaba huo wa nyumba za askari katika Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro uko maeneo yote ikiwemo Same, Rombo, Moshi Vijijini, Siha na Mwanga. Je, ni nini hasa mkakati wa Serikali kuwapatia maafisa hawa wa polisi nyumba maeneo yote hayo? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa watu hawa wanashinda mchana wote kazini na jioni tu ndiyo wanaonekana nyumbani, familia huwa hazina mahali palipo na utulivu na watoto wao/wanafunzi wanakuwa na shida sana ya kujisomea.

Je, kuna mpango wowote wa kujenga vituo vya watoto hao wa askari hawa vya kujisomea maeneo ya nyumbani *(recreation centers)*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongelea habari ya uhaba wa nyumba za askari katika wilaya zote za Mkoa wa Kilimanjaro; Same, Rombo, Siha pamoja na Mwanga. Serikali inatenga fedha kila mwaka na tunajenga nyumba hizi awamu kwa awamu. Kwa hiyo, wilaya hizi alizozitaja pia zitaingizwa kwenye mpango awamu kwa awamu zitajengwa nyumba za askari wetu ili waweze kukaa katika mazingira ambayo ni salama kwa ajili ya utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwa kuwajengea watoto hawa maeneo ya kuchezea kwa kweli sasa hivi Serikali haina mpango huo. Pengine huko mbele ya safari tutaangalia, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, Wilaya ya Mbulu ni wilaya kongwe nchini, makazi ya askari polisi katika wilaya hiyo ni chakavu sana. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kwenda kujenga upya makazi hayo ya askari polisi katika Wilaya ya Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mji kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba nyumba zote za askari zinakuwa ni nzuri na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge halmashauri inasimamia, mara nyingi nyumba za askari za Wilaya ya Mbulu ni chakavu ni kweli, na tutaziweka kwenye mpango na kutengewa fedha ili tuweze kuzikarabati, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Jimbo la Mbulu Vijijini Kituo cha Polisi Yaeda Chini wananchi wamekijenga kwa nguvu zao na mmeleta polisi, lakini polisi wale hawana kabisa nyumba za kukaa. Je, ni lini mtaleta fedha ili polisi wakajengewe nyumba katika Bonde la Yaeda Chini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Yaeda Chini kwa ujenzi wa kituo cha polisi katika eneo hilo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kazi hii kubwa iliyofanyika Serikali itaunga mkono juhudi hizo na kuweka kwenye mpango wa kujenga nyumba za askari wetu ili waweze kufanya kazi katika mazingira safi na salama, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunao wageni wa Mheshimiwa Spika, wageni nane wa Mheshimiwa Spika ambao ni Uongozi wa Taasisi ya Lete...

Mheshimiwa Waziri wewe nenda tu.

Wageni nane wa Mheshimiwa Spika ambao ni Uongozi wa Taasisi ya Lete Mabadiliko Chanya Ulipo (LEMACHU) kutoka Jijini Mbeya, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya ambaye ni mwanae, katika wanafunzi waliokuja Bungeni leo kutoka *Leadership Primary School,* mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri yupo kwenye kundi hilo, simama tukuone. *(Makofi)*

Tunao wageni 130 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, Viongozi wa Jamii ya Wafugaji kutoka Wilaya ya Longido Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Cosato David Chumi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mke wake, Ndugu Esther Mbezi. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ndugu Gaudensia Masini, mfanyabiashara kutoka Kariakoo Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ndugu zake kutoka Mkoani Dodoma na Mbeya. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Felister Deogratius Njau, jamaa zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga, rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, watoto wake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 23 na walimu wawili wa Shule ya Sekondari Wella kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 18 kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania wanaotarajia kushiriki mafunzo ya uongozi ya *Mandela Washington Fellowship 2025* yaliyo chini Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Siasa Ubalozi wa Marekani, Ndugu Richard Allen, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 na Walimu watano wa Shule ya Sekondari Kihesa kutoka Mkoani Iringa, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 74 na viongozi 10 ambao ni Wanachama wa Skauti kutoka Shule ya Sekondari *Peace and Love* na Shule ya Msingi *Siha Leadership* zilizopo Wilaya ya Hai, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Munira.

Na. 461

**Migogoro ya Ardhi Kati ya Wakulima na Wafugaji**

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza niombe uniruhusu nitoe shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutupitishia bajeti jana na sasa tunaingia kazini kwa ajili ya kwenda kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa migogoro ya muingiliano kati ya wakulima na wafugaji katika maeneo mengi hapa nchini. Katika kukabiliana na tatizo hilo Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kama kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango wa Matumizi Bora ya Ardhi, kutoa elimu juu ya wananchi kubainisha maeneo ya wafugaji na wakulima katika maeneo yao kupitia viongozi wa maeneo hayo kwa maeneo yale ambayo hayajawekewa mpango wa matumizi bora ya ardhi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuwakumbusha wananchi kuhakikisha kuwa wanatumia ardhi kuendana na mipango ya matumizi iliyopangwa ili kuondoa muingiliano wa matumizi ya ardhi ambayo imekuwa ni chanzo cha migogoro ya wakulima na wafugaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninapenda kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanga na kumilikisha vijiji nchi nzima ili kuondoa migogoro hii ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji?

Swali langu la pili, kuna wawekezaji wenye mashamba na maeneo makubwa ya ardhi ambayo mashamba haya hayajaendelezwa hadi sasa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufuta hati hizi ili kurejesha maeneo haya kwa wananchi ili waweze kupata kulima na kufuga? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Munira kwa maswali yake ya msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili la kupanga na kumilikisha ardhi hapa nchini kupitia Tume yetu ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ni zoezi endelevu na linategemea upatikanaji wa fedha na hata hivi nia ya Wizara ni kuendelea kupima kwa kasi kubwa ili kuhakikisha kwamba vijiji hivi vinabainisha maeneo mbalimbali ya matumizi kwenye maeneo yao ili kuepusha migongano hii ambayo inajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kusema kwa ufupi kabisa niipongeze Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mkakati wake wa kuja kuwaweka pamoja wafugaji kwa sababu sasa hivi wafugaji wengi wanazunguka. Sasa hivi wameshamaliza Tanzania nzima na sasa wako mpakani mwa nchi jirani kama Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tusiwapoteze hawa na Wizara yangu ambayo itakwenda kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Kilimo na TAMISEMI, tukae pamoja tuwe na wazo moja juu ya kuhakikisha wafugaji hawasambai sambai hovyo hovyo kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la mashamba Mheshimiwa Munira kama ulikuwa unatusikiliza jana wakati wa wasilisho la bajeti yetu tumezungumzia suala la mashamba makubwa ambayo mengine yametelekezwa. Tumeunda timu ya pamoja katika kuyafuatilia mashamba haya na pale tutakapokwenda kuyabainisha mashamba ambayo hayana uendelevu wowote ushauri wako utazingatiwa katika kuhakikisha kwamba tunarudisha ardhi hii mikononi mwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itamaliza mgogoro kati ya wananchi wa Korotambe na Magwe, Nyamerambaro na Malaspora, lakini vilevile mgogoro wa wananchi na Hifadhi ya Serengeti kule Tarime Vijijini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba kwa sasa tunaenda kwa kasi kubwa kupitia maeneo ya vijiji kuyawekea mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo tumeona limekuwa suluhisho kubwa sana la migogoro hii ambayo inatengeneza muingiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waitara katika mazingira ya kawaida hata hili la mpaka na Hifadhi yetu ya Serengeti tunakwenda kulisimamia ili wananchi hawa waishi bila migogoro yoyote na tunakushukuru sana Mheshimiwa Waitara umekuwa mfuatiliaji mzuri wa migogoro hii ya wafugaji walioko kwenye mipaka yetu na hifadhi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nilitaka kufahamu ni nini mkakati wa Serikali ili kuweza kutatua mgogoro uliopo wa kimipaka kati ya Halmashauri ya Wilaya ya *Masasi DC* na Halmashauri ya Wilaya ya *Newala DC*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hii migogoro ya kimipaka nchi yetu ilishapimwa siku nyingi sana isipokuwa tu kinachojitokeza kinakuwa na maslahi, unaweza ukasema kama maslahi binafsi kwa sababu wilaya na wilaya mipaka yake inajulikana kwa muda mrefu sana na wakati mwingine migongano hii inatokana aidha na mazao yanayolimwa miongoni mwao, wakurugenzi wengi wanapigani hili likauzwe huku hili likauzwe huku.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambe ninadhani baada ya hapa tukutane tujue msimamo halisi wa mgogoro huu umekaaje kwa sababu tayari nchi ilishapimwa yote na hatuna migoro mikubwa sana kati ya wilaya na wilaya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Ntara.

Na. 462

**Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Waliopo kwenye Programu za *BBT***

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza: -

Je, hadi sasa wanafunzi wangapi kutoka vyuo vikuu vya kati wapo katika programu za *BBT*?

**NAIBUSPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza miradi mitano ya Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora ambapo vijana 120,111 wamenufaika moja kwa moja kupitia programu hiyo kupitia Wizara ya Kilimo, sekta binafsi na wadau wa maendeleo. Kwa upande wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zake Programu ya *BBT* ina jumla ya vijana 1,919; kati ya hao, vijana 1,558 ni wahitimu wa mafunzo kupitia vyuo vikuu vya kati na vijana 361 ni wahitimu wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vijana 1,558 ambao ni wahitimu wa vyuo vikuu vya kati nchini, vijana 210 wanajishughulisha na kilimo katika mashamba makubwa ya pamoja ya Chinangali na Ndogowe yaliyopo katika Wilaya ya Chamwino, Mkoani Dodoma; vijana 1,348 wako kwenye Mradi wa *BBT* – Ugani unaojihusisha na utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wadogo, ambapo vijana 740 wanajishughulika na zao la pamba, 500 zao la korosho na 108 zao la kahawa.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri majibu yako yanaleta tumaini umejibu vizuri sana.

Sasa katika kuongeza ajira, je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza *BBT* katika eneo hilo la kilimo ili kuwe na *BBT* kuchakata, *BBT* masoko na *BBT* mauzo ili kuongeza hizo ajira? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ntara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, *program* ya *BBT* ina miradi mitano, katika maeneo aliyoyataja *value addition* ni sehemu mojawapo ya Mradi wa *BBT* na tunao vijana katika maeneo ya alizeti ambao wamepewa fedha kupitia mradi wa *BBT* na wanaongeza thamani katika Mkoa wa Singida na maeneo mengine. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe na baadae Mheshimiwa Profesa Patrick.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Hai tumeweka maeneo mbalimbali tengefu kwenye Kata ya Weruweru, Kata ya Rundugai kwa ajili ya kuanzisha Programu ya *BBT;* ni mpango gani Serikali ilionao kwa ajili ya kuanzisha *BBT* Mkoa wa Kilimanjaro, hususan Wilaya ya Hai? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma bajeti ya Wizara ya Kilimo, mwaka huu tumesema kwamba Programu ya *BBT* inahamia katika ngazi za halmashauri, tunaiomba tu halmashauri yako i-*communicate* na Wizara ya Kilimo rasmi kwamba wametenga maeneo kwa ajili ya programu hiyo na tutakuja kuweza kuwasaidia, kuweza kutekeleza kwa ajili ya vijana wa Wilaya ya Hai. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Profesa Patrick.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Moshi hasa Halmashauri ya Moshi ina uhaba mkubwa wa ardhi na tuna vijana wengi ambao wangependa kushiriki katika programu hii ya *BBT*. Je, Serikali inasemaje kuhusu maeneo haya yenye uhaba wa ardhi ili vijana waweze kushirikishwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kuwa ni kweli Mkoa wa Kilimanjaro una uhaba wa ardhi lakini ni ukweli vilevile Mkoa wa Kilimanjaro una ardhi ambayo iko chini ya Vyama Vikuu vya Ushirika na haitumiki. Kwa hiyo, kama Wizara tumeongea na Mkuu wa Mkoa na hivi karibuni tunaunda timu kwenda kufanya tathmini ardhi zote zilizopo chini ya Vyama Vikuu vya Ushirika na watu wote walioingia mikataba ya muda mrefu ambao hawaendelezi tutazichukua hizo ardhi na kuzirudisha chini na Vyama Vikuu vya Ushirika ambavyo vina tabia ya kukimbilia mahakamani, tutavifuta na kuviondoa katika Mkoa wa Kilimanjaro tutaanza upya kujenga ushirika ambao una maslahi ya wananchi na siyo viongozi wachache. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Mbogo.

Na. 463

**Ujenzi wa Ghala Kata ya Chala - Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga ghala katika Kata ya Chala kwani kuna wakulima wengi wa zao la mahindi na hawana sehemu ya kuhifadhia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi ni moja ya Wilaya muhimu katika uzalishaji wa chakula nchini. Katika mwaka 2024/2025 uzalishaji wa mazao ya chakula katika wilaya hiyo ulikuwa tani 688,352, kati ya hizo tani 44,073 zilizalishwa katika Kata ya Chala. Hivyo, kutokana na umuhimu wa Kata ya Chala katika kuchangia upatikanaji wa chakula nchini, Wizara katika mwaka fedha 2025/2026 imepanga kujenga ghala katika kata hiyo kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna na likiwa ni ombi la Mbunge wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaishukuru Serikali sana kwa majibu mazuri na wananchi wa Kata ya Chala wamefurahi sana kwa ujenzi wa maghala katika Kata ya Chala. Kata ya Nkandasi na Kata ya Myula nazo zina changamoto ya maghala kwa kuhifadhia mazao.

Je, ni lini Serikali itaenda kuwajengea maghala? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Nkasi kwa maana ya Nkasi Wilaya zote mbili, Kusini na Jimbo lile lingine ni maeneo ya uzalishaji. Niwaombe tu taratibu kutokana na uwezo wa kifedha Serikali itaendelea kujenga maghala. Lengo la Serikali ni kuwa na uwezo wa uhifadhi wa tani 3,000,000 tumeshafika tani 700,000 sasa hivi kutoka 250,000. Kwa hiyo, tunaamini siyo muda mrefu tutaendelea kufanya tathmini, fedha zinapopatikana tutaendelea kujenga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, ukanda ule wa kule Ziwa Victoria ni Mkoa wa Shinyanga tu ndiyo kuna ghala la *NFRA,* lakini wananchi wa Mkoa wa Mara wao wanalima sana. Sasa ni lini Serikali itahakikisha kwamba, inajenga ghala walau kule Mkoa wa Mara nao waweze kuhifadhi haya mazao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimhakikishia Mheshimiwa Matiko, nimhakikishie Profesa Mkenda, nimhakikishie Mbunge wa Mkinga na watu wote walioko kwenye *border* za Tanzania na nchi zinazotuzunguka kwamba kwenye bajeti mliyotupitishia kwenye Bunge hili tunajenga masoko na maghala kwenye *border* ili kuweza ku-*facilitate trade*. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunajenga soko jipya Wilaya ya Tarime ukiacha hili

linaloendelea sasa hivi na tutajenga ghala *border* kwa ajili ya kusaidia biashara ya mazao na nchi zinazotuzunguka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Ngassa.

Na. 464

**Mradi wa Maji Ziwa Victoria kwenda Igurubi**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, lini mradi wa usambazaji maji ya Ziwa Victoria kutoka Bulenya kwenda Igurubi utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na upanuzi wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kutoka Kijiji cha Igogo kwenda Igurubi, Wilayani Igunga Mkoa wa Tabora. Kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tanki moja lenye ujazo wa lita 1,000,000, uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 150 sanjari na ujenzi wa vituo 57 vya kuchotea maji. Mradi huo utekelezaji wake umefikia 60% na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2025 na kunufaisha wananchi 71,726 waishio kwenye vijiji 18 vilivyopo kwenye kata saba za Mwamashiga, Mbutu, Isakamaliwa, Kining'inila, Mwamakona, Igurubi na Kinungu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, kwanza, nianze kumpongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso kwa *commitment* kubwa ambayo unaifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika miradi ya maji ya kumtua mama ndoo kichwani, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anakumbuka kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mliweka *commitment* kwamba maeneo ambayo tayari bomba limepita kwa mfano kule Mwamashiga, Mbutu, Mwamakona tayari mlitakiwa watu wafungue maji yaanze kutoka kwa ajili ya wananchi kutumia na kwa kuwa mkandarasi ameshalipwa zaidi ya 50% ya fedha alizoingia kwenye mkataba na Serikali.

Je, nini kauli ya Serikali katika hili kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Igunga wanaanza kutumia maji haya ambayo tayari fedha zimekwenda na maeneo mengi wameshatandazwa lile bomba? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mradi umejengwa na baadhi ya maeneo yamekamilika, maelekezo ambayo tuliyatoa na ndiyo msimamo wa Serikali ni kuhakikisha wananchi wale wanapata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini mradi wa kimkakati wa maji toka Bonde la Mto Rufiji kuelekea Wilaya za Rufiji, Kilwa na Liwale utaanza kutekelezwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Wizara ya Maji kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kutumia rasilimali toshelevu ikiwemo Mto Rufiji na maeneo mengine ili kuhakikisha kwamba, inatatua matatizo kwa kiwango kikubwa. Sasa hivi tumempata Mhandisi Mshauri na yuko kazini kwa ajili ya tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimhakikishie baada ya tathmini, utafutaji wa fedha utapatikana kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma nilikuona umesimama.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Kata ya Masoko ambayo ipo kwenye Wilaya ya Rungwe utakamilika, mradi huo unategemewa na vijiji 15? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Tunapata faraja ya Mheshimiwa Rais kupitia bajeti yetu ya Wizara ya Maji, tumeongezewa fedha zaidi ya shilingi trilioni moja kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutoa fedha kuhakikisha miradi hii inakamilika na wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya na hasa katika ule mkutano wa jana, tunampongeza sana, lakini pili nimpongeze vilevile Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba tulipata pesa nyingi shilingi bilioni 12.4 na ile ilikuwa ni awamu ya kwanza; je, lini utatupatia fedha za kukamilisha ule mradi awamu ya pili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Mama yangu Salma Kikwete kwa kweli eneo la Mchinga lilikuwa na changamoto kubwa sana ya maji, hata ukichimba visima, maji yalikuwa hayapatikani, lakini tunayo dhamira ya dhati kuyatoa

maji Lindi Mjini yamefika mpaka Mchinga. Nataka nimhakikishie kwamba safari moja huanzisha nyingine, tumeianza safari ya kwanza kuyaleta maji Mchinga, tunakwena *phase II* kuhakikisha na maeneo mengine yanaenda kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali imekuwa na miradi ya kupeleka maji mikoa mbalimbali kutokea Ziwa Victoria, Wilaya ya Kyerwa na Karagwe ni kilometa 80 tu kwa barabara kutoka Ziwa Victoria, lakini wananchi wake hawa hawana maji na maeneo mengi wanapojaribu kuchimba maji hayapatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua nini msimamo wa Serikali kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Wilaya za Kyerwa na Karagwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo uelekezo wa Wizara ya Maji na ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba tuende katika uelekeo wa *national building*. Nchi yetu ya Tanzania si maskini wa vyanzo vya maji, tuna mito mikubwa, tuna maziwa makubwa, kwa hiyo huo ndio uelekeo wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na hata dhamira ya Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti, tutakwenda katika uelekeo huo katika kuhakikisha tunatumia maziwa na mito mikubwa kuhakikisha maeneo mbalimbali yanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Waziri yuko tayari kutuletea fedha za dharura ili tuweze kusambaza maji Kijiji cha Muheru, Bassodesh na Getamock

ambapo mabomba tayari yamefika muda mrefu pale na wananchi wanasubiri huduma ya maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, faraja ya Waziri wa Maji ni watu wapate maji. Ninakuomba Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa mabomba yameshafika tukutane kwa haraka tuone namna gani ya kuweza ku-*support* hilo ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Shangazi.

Na. 465

**Sekta Binafsi Kuwekeza katika Miundombinu ya Reli *SGR***

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha taratibu za kisheria ili kuruhusu sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya reli ya kisasa - *SGR?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha marekebisho ya Sheria ya Reli Na. 10 ya Mwaka 2017 ili kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma ya usafirishaji kupitia njia ya reli, ambapo marekebisho ya kanuni za uendeshaji yalitangazwa kwenye Gazeti la Serikali mwezi Januari, 2025. Kwa sasa *TRC* inaendelea na ukamilishaji wa taratibu kwa ajili ya kuanza uendeshaji kupitia sekta binafsi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Wizara hii ya Uchukuzi ndiyo ambayo pia inasimamia meli zilizoko katika maziwa yetu makuu hapa nchini, pia inasimamia reli ya *TAZARA*.

Je, haioni kwamba ni muhimu pia kubadilisha sheria za sekta hizo mbili nilizozitaja ili na kwenyewe turuhusu sekta binafsi iweze kushiriki katika kukuza uchumi pia kurahisisha huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

Swali la pili, zipo baadhi ya sekta za uchukuzi ambazo hazisimamiwi na Wizara hii ya Uchukuzi, kwa mfano, usafiri na usafirishaji katika Jiji la Dar es Salaam kupitia kampuni ya *DART*. Miundombinu ya *DART* ipo, lakini watoa huduma wamekuwa kero kwa wananchi kiasi kwamba wanatumia muda mrefu sana kupata huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.

Je, Serikali kupitia Wizara hii ya Uchukuzi iko tayari kukaa na watu wa TAMISEMI na kuweza kuwapa mipango madhubuti ya kuiruhusu sekta binafsi iingie katika miundombinu ya *DART* ili waweze kutoa huduma katika miundombinu ile? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru na nimshukuru Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa maswali yake ya nyongeza pamoja na pongezi ambazo amezitoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana naye kwamba uelekeo wa Serikali kwa sasa ni kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa uchumi wa Taifa letu na hii ni kwa sababu Serikali haiwezi wakati wote ikawa inajenga miundombinu na kisha inaleta vitendea kazi, tunaposhirikisha sekta binafsi tunaongeza ufanisi pamoja na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ametoa ushauri na ameuliza kwenye upande wa *TAZARA* na kwenye meli, kwa ujumla kwenye bandari. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imekwishaona umuhimu wa jambo hili na kupitia Sheria ya Reli ya Tanzania na Zambia, Sura 143 iliruhusu ushiriki wa sekta binafsi na hivi navyozungumza tayari makampuni mawili yanafanya kazi na lipo kampuni la tatu ambalo pia nalo linatarajiwa kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tumeruhusu mfumo huu, mwaka wa fedha peke yake uliopita wa 2023/2024 kati ya tani 447,000 tumeona 73% ya mzigo uliosafirishwa kwa *TAZARA* yaani tani 328,000 umesafirishwa na hawa wenzetu wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sheria zingine kama Sheria ya Bandari, Sura ya 166 tumeruhusu wawekezaji binafsi na tumeona wenzetu wa *DP World* pamoja na makampuni mengine walipoingia, tumeshuhudia mapato ya kikodi yameongeza kutoka shilingi trilioni saba mpaka shilingi trilioni nane, uhudumiaji wa shehena umeongezeka kutoka makasha 17,000 mpaka 25,000 pamoja na maeneo mengine. Pia kupitia Sheria ya Uwakala wa Meli Sura ya 415 tumeshuhudia pia sasa kwenye maziwa yetu makuu wawekezaji binafsi wanaruhusiwa na wanafanya shughuli zao kwa maana ya kuendesha meli kwenye Ziwa Tanganyika pamoja na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia namna ya kuboresha miundombinu kama *DART,* je, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi tuko tayari kushirikiana na wenzetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye pia ni Katibu wa Wabunge wa CCM hapa Bungeni kwamba Serikali ni moja, tumepokea ushauri wake na sisi sekta ya uchukuzi chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa tuko tayari kukaa na wenzetu kushirikishana uzoefu pale itakapohitajika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nilitaka Mheshimiwa Waziri atupe kwa kifupi katika hii miaka minne ya Mama Samia, kwa sababu tunajua *SGR* inajengwa kwa vipande. Ni vipande vipi vimekamilika katika miaka hii minne na tujiandae vipi wawekezaji binafsi kuwekeza katika hivyo vingine kwa muda upi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Jesca kwa sababu anafuatilia kwa ukaribu kazi kubwa iliyofanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan katika miaka hii minne. Sote ni mashahidi kwamba, ndani ya miaka hii minne, Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuta vipande viwili yaani kipande cha kwanza cha Dar es Salaam mpaka Morogoro na mpaka hapa Dodoma, Makutupora, ameongeza vipande vingine vitano kutoka hapa kwenda mpaka Mwanza na mpaka Kigoma. Alikuta kilometa 722 zinajengwa akaongeza kilometa 1,540 na kufanya kilometa 2.228.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, alikuta fedha zilizolipwa ni shilingi trilioni nne tu, lakini katika miaka hii minne ameongeza trilioni saba na kufanya jumla ya shilingi trilioni 11. Kwa hiyo, unaweza kuona fedha alizolipa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni 63% ya fedha zote ambazo zimelipwa katika mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, hapo nyuma tulikuwa tumejenga *TAZARA (cap gauge)* tulikuwa tumejenga reli ya *meter gauge* mpaka Mwanza na Kaskazini, lakini bado nchi yetu ilikuwa haijawahi kuaminika katika diplomasia ya miundombinu kwamba nchi zingine zituombe tukawasimamie. Hivi navyozungumza tayari Tanzania imeaminika na wenzetu wa Burundi tunasimamia ujenzi wa reli yao. Kwa hiyo, upekee wa Dkt. Samia kama ambavyo mmesikia hata jana kwenye Mkutano Mkuu wa CCM wakizungumza kazi kubwa iliyofanyika, kwa kweli ni wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza kwa kazi kubwa na kwamba sisi kama

sekta na tuliopewa dhamana ya kusimamia sekta hii, tunajipanga vizuri kuhakikisha kwamba sheria hii ya *open access* ya kushirikisha wawekezaji binafsi inapewa nguvu zaidi na watu wanashirikishwa ili wajiandae kuja kuleta vitendeakazi kwenye miundombinu hii mizuri ambayo itakuwa imeshakamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Serikali ilituambia itajenga Reli ya Kusini kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay kwa ubia. Nataka kujua, imefikia hatua gani katika utekelezaji wa mradi huo ambao ni muhimu sana kwa sisi watu wa Kusini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nimjibu Mheshimiwa Tunza Malapo kwa swali lake alilouliza ambalo linaulizwa mara kwa mara na Waheshimiwa Wabunge wa Kusini wote na Watanzania kwamba ni lini mtajenga reli yetu ya kutoka Mbamba Bay mpaka Mtwara ambayo ni Reli ya Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa ujenzi wa reli hiyo, kwanza, kutokana na sababu za kihistoria kuwaenzi wazee wetu; lakini pili ikiwa ni kuunganisha uchumi kati ya Bahari ya Hindi kupitia Bandari ya Mtwara pamoja na Bandari yetu ya Mbamba Bay.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishaanza kufanya baadhi ya hatua. Hivi ninavyozungumza tumejenga Bandari ya Mtwara ambayo ni pale Kisiwa Mgao kwa ajili ya kusafirisha bidhaa chafu ili kutoa makaa ya mawe kule Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga Bandari yetu ya Mbamba Bay ambayo tayari mkandarasi yuko *site* na tayari tumekwishaanza hatua za kutafuta fedha. Lengo tukishapata fedha kwa mfumo wa ubia tuanze kuijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Tunza Malapo kwamba avumilie kidogo kwa sababu kama nilivyotoka kujibu swali la msingi na maelezo ya ziada kwamba tunajenga kilometa zaidi ya 2,200. Hebu tuzimalize kwanza hizo wakati huu pia tunapambana tufike hatua fulani nzuri kisha tuweze kuanza na upande huu mwingine ambao umeusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu fedha pekee inayotumika katika ujenzi wa hizi zaidi ya kilometa 2,000 ni takribani shilingi trilioni 28 mpaka 30 na sehemu yake tunazikopa na ndiyo maana kuna baadhi ya wenzetu wanauliza Serikali hii inakopa sana. Tunakopa tukajenge miundombinu ya kiuchumi inayokwenda kutuzalishia maradufu zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Bupe.

Na. 466

**Changamoto ya Usafiri Ziwa Tanganyika**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya usafiri katika Ziwa Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya usafiri iliyopo katika Ziwa Tanganyika. Katika kupata ufumbuzi wa changamoto hii, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Serikali inaendelea na ukarabati wa meli ya MT. Sangara na imeanza kufanya kazi mwezi Mei 21, 2025.

(ii) Serikali inaendelea na ukarabati wa Mv. Liemba katika Ziwa Tanganyika ambapo ukarabati wake umefikia 15%.

(iii) Aidha, Serikali ilisaini mkataba na Kampuni ya *Songoro Marine* kwa ajili ya kukarabati Meli ya Mv. Mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imemlipa mkandarasi kiasi dola za Kimarekani 8,800,000 kama sehemu ya malipo ya awali *(advance payment)* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli. Kukamilika kwa miradi hii kutapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya usafirishaji majini katika Ziwa Tanganyika na hivyo kuchochea uchumi kwa wananchi wa mwambao wa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kabisa ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na ninashukuru kwa kuanza kwa Mv. Sangara, meli ya mafuta, tunashukuru sana Wana-Rukwa tunashukuru, tunaipongeza sana Serikali. Pia tunashukuru kwa ukarabati unaoendelea wa meli. Pamoja na pongezi hizi nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza lingine ni ushauri; je, Serikali haioni umuhimu wa kushirikiana na wenzetu wa Kongo kukarabati bandari zetu ikiwemo Bandari ya Kalemie na Moba na hizi bandari zetu zikarabatiwe ili meli zetu zitakapokamilika ziweze kufanya kazi vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga fedha ya kujenga meli kubwa katika Ziwa Tanganyika ili *SGR* itakavyoanza iweze kufanya kazi vizuri? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata kwa sababu amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana na wa karibu wa maendeleo katika Mkoa wa Rukwa lakini pia kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, nilitaka kwenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba kutokana na umuhimu mkubwa wa Ziwa Tanganyika, Serikali imekwishasaini makubaliano kati ya Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Kongo ili kuhakikisha kwamba bandari zilizopo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika zinaboreshwa na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari katika hatua za awali wenzetu wa Kongo wamekwishasaini mkataba pamoja na kampuni moja ya kichina ambayo imekwishaanza kujenga Bandari ya Kalemie *(New Kalemie Port)*. Bandari hiyo, wenzetu hao wanafanya kazi hiyo sambamba na kujenga barabara ya lami kutoka pale Kalemie mpaka Manono ambapo wanakusanya madini mbalimbali ikiwa ni pamoja na *lithium, gold* na vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kampuni hiyo hiyo ndiyo inajenga meli nne katika Ziwa Tanganyika ambazo zitakuwa na uwezo wa kubeba tani 2,000. Hizi meli nne zitakamilika mwakani mwezi Julai kwa maelezo waliyotupatia na yeye Mheshimiwa Bupe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanaopakana na Ziwa Tanganyika tumekwenda pamoja kushudia kazi kubwa iliyo nzuri. Yote hiyo, inatokana na makubaliano ambayo Serikali tumeyafanya na hao wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ujenzi wa bandari hiyo, tayari tupo kwenye hatua za upembuzi yakinifu kushirikiana na wenzetu kutazama fursa zilizopo kwenye Bandari ya Moba, lakini upande wa kwetu tayari tulishakamilisha ujenzi wa bandari kama Kasanga, Kalema pamoja na zingine ambazo zipo katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha swali lake la pili kuhusiana na ujenzi wa meli; kama ambavyo nimezungumza kwenye swali la

msingi; cha kwanza tumeanza kukarabati meli zote za kihistoria ambazo zilikuwepo kwenye Ziwa Tanganyika na kwa sehemu kubwa zimeanza kufanya kazi kama hii ya MT Sangara na Mwongozo ambazo zinaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hivi ninavyozungumza tumesaini mikataba kama miwili au mitatu. Mkataba wa kwanza ni wa kujenga meli kubwa ya tani 3,500. Meli hii itakayojengwa itakuwa ndiyo meli kubwa kuliko meli zote ambazo zinajengwa sasa hivi katika maziwa makuu yote nchini; hiyo inajengwa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi tunakwenda kujenga meli nyingine ya tani 400 na itakayobeba abiria 600; zote zitajengwa Ziwa Tanganyika. Haya ni maandalizi mazuri kwamba itakapokamilika *SGR,* mzigo ukitoka Bandari ya Dar es Salaam ukipita kwenye reli yetu ukifika pale Kigoma uweze kusafirishwa kwenda upande wa pili na hivyo tuweze kuona manufaa ya kiuchumi makubwa ya uwepo wa miundombinu hii katika nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Habari, Utamaduni, Mheshimiwa Kamamba.

Na. 467

**Ujenzi wa Uwanja wa Michezo – Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga uwanja wa michezo katika Wilaya ya Kakonko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na viwanja vya michezo katika kila wilaya, ikiwemo Wilaya ya Kakonko ili kuibua na kukuza vipaji, kuimarisha afya za wananchi pamoja na kuchochea uchumi kupitia sekta ya michezo. Ingawa kwa sasa Wilaya ya Kakonko haijajumuishwa kwenye miradi ya moja kwa moja ya Serikali ya ujenzi na ukarabati wa viwanja kwa ajili ya *CHAN* na *AFCON*, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ikishirikiana na TAMISEMI inaendelea kutoa miongozo na ushauri wa kitaalam kwa halmashauri zote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko katika kutenga maeneo na bajeti kwa ajili ya ujenzi wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuzihimiza halmashauri zenye nia ya kujenga viwanja vya michezo, ikiwemo ya Kakonko kuanza mchakato wa ndani wa upatikanaji wa ardhi, kutenga fedha kwenye bajeti zao na kuwasilisha maombi rasmi Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ajili ya kupata msaada wa kitaalamu na kiufundi ili kuhakikisha dhamira ya kuwa na viwanja vya michezo nchini kote inatimia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali; kwa majibu ya Serikali hofu yao ni Wilaya kutokuwa na ardhi na kwa nafasi hii nithibitishe kwamba sisi Kakonko ardhi tunayo, tatizo ni fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huu. Ombi na swali, lini Serikali sasa itatuletea fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa sababu ardhi tunayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, lengo la kuomba kujengewa kiwanja ni kuibua vipaji vya vijana wetu katika Wilaya ya Kakonko. Mimi kama Mbunge nimeanzisha ligi inaitwa *Kamamba Cup* kwa nia moja ile ile ya kuibua vipaji. Je,

Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutuletea wataalam kwa ajili ya kubaini vijana wetu ambao wanaendelea na ligi hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, kwanza niwapongeze Halmashauri ya Kakonko wakishirikiana na Mbunge Mheshimiwa Aloyce Kamamba kwa kuwa na utayari wa kutengeneza miundombinu ya michezo kwenye halmashauri yao kwa kuanza kwa kutenga maeneo. Kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni kwenye miundombinu itakayotumika kwa ajili ya *CHAN 2025* na *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa hatua mbayo Kakonko wameifikia nimuombe Mheshimiwa Mbunge wawasilishe rasmi maombi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kupata msaada wa kitaalam na kiufundi na hali ya rasilimalifedha itakaporuhusu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutashirikiana nao katika kuhakikisha tunajenga miundombinu ya michezo kwenye halmashauri yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuanzisha *Kamamba Cup* kwa ajili ya kugundua na kulea vipaji pale kwenye Halmashauri yake ya Kakonko. Ninamuomba Mheshimiwa Mbunge nikimaliza hapa tukutane anipatie ratiba ya *Kamamba Cup* na mimi nitakuwa tayari kumtumia wataalam kutoka Shirikisho la Soka Tanzania kwa ajili ya kwenda kung'amua vipaji vinavyopatikana pale Kakonko.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika nitaangalia na timu zilizopo karibu, ninafikiri ni Mashujaa wako karibu pale nitawaomba na wao pia wapeleke skauti wao ili tuone kama Kakonko inaweza kutoa wachezaji kwa ajili ya kucheza kwenye timu yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mzeru.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujenga na kuboresha viwanja vya michezo nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kuboresha viwanja vya michezo mashuleni na vyuoni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mzeru. Kwa sasa mpango ambao Serikali inao ni kutengeneza shule mbili za michezo katika kila mkoa, ambapo tuna jumla ya shule 56 na mwaka huu wa fedha tayari tumepata fedha kwa ajili ya kuanza kutengeneza shule saba za michezo ambapo tunachofanya ni kwenda katika shule za sekondari ambazo zipo na tunatengeneza viwanja kwa ajili ya michezo yote ikiwemo mchezo wa mpira miguu, mchezo wa *netball, basketball, volley ball* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo tutakapokamilisha mradi huu tutakuwa na shule 56 nchini kote ambazo zina viwanja vya michezo na hii ni kuhakikisha kwamba tunaunga mkono na tunatekeleza kwa vitendo maono ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha miundombinu ya michezo inatapakaa nchini kote, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Halmashauri yetu ya Mji wa Babati tumejenga uwanja mzuri kabisa wa Tanzanite Kwaraa na ni miongoni mwa viwanja vinavyofanya vizuri. Tumeleta maombi ya viti kwenu Wizarani mtu-*support* na ukizingatia kesho Simba na *Big Stars* wako Babati. Ni lini mtatupatia hivyo viti Mheshimiwa Naibu Waziri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Gekul.

Mheshimiwa Naibu Spika, viti anavyovizungumzia Mheshimiwa Mbunge Gekul ni viti ambavyo tulikuwa tunavitoa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. Kama unavyofahamu, miongoni mwa maeneo ambayo tunayafanyia ukarabati ni kubadilisha viti vyote 63,000 ambavyo viko katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viti vile kama unavyofahamu viliwekwa mwaka 2007, kwa hiyo, vingi kati yao vimeharibika. Tunachofanya sasa hivi tuko katika hatua ya mwisho ya kutoa viti vyote ili tujue tuna idadi gani ya viti na kutokana na maombi mengi ambayo tunayo tutaona tunaweza kugawa viti vingapi vingapi kwa kila ombi ambalo limetufikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Gekul maombi yake tunayo na tutahakikisha Uwanja wa Tanzanite nao unapata baadhi ya sehemu ya viti hivi na kuhakikisha wapenzi wa mpira wa miguu wanaohudhuria pale wanaweza kuvikalia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Usonge, wajiandae Mheshimiwa Kasaka na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ndogo ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile vijana wengi wamejiajiri kutokana na uwekezaji mzuri wa soka, lakini zipo baadhi ya changamoto; je, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha kabisa inatanua wigo ili vijana wengi waweze kupata ajira hususan kwenye michezo hii ya kubahatisha? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Serikali ambayo inashiriki kwenye swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge ni ku-*regulate* na kuhakikisha sheria za nchi zinafuatwa, hazikiukwi, lakini halikadhalika kunakuwa na athari chanya kwenye ushiriki wa vijana kwenye michezo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo unafahamu kuna changamoto nyingi, *addiction* ambazo vijana wengi wanaingia kwa kushiriki michezo hii na Serikali jukumu lake ni kuhakikisha wanashiriki na kunufaishwa na michezo hii bila kupata *addiction* ambazo pengine zingeweza kuathiri maisha yao moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali inaendelea kufuatilia kwa ukaribu kuhusiana na ushiriki wa vijana kwenye michezo hii lakini hali kadhalika kutengeneza *platforms* mbalimbali ili kuhakikisha wanashiriki na kunufaika bila kuathiriwa na michezo ambayo wanashiriki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Mheshimiwa Festo.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa kushirikiana na wadau tunaendelea na ujenzi wa uwanja wa michezo na mpaka sasa tumefikia hatua nzuri na tumeshaagiza nyasi bandia.

Je, upi mpango wa Serikali kuweza kutuunga mkono kutuletea fedha ili tuweze kujenga majukwaa na uwanja huu uweze kuisha kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu kwenye swali la msingi, hali ni hiyo hiyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya. Kwa sasa kipaumbele kipo kwenye

miundombinu ya michezo itakayotumika kwa ajili ya michezo ya *CHAN 2025* na *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Kasaka na Halmashauri ya Chunya waweke maombi rasmi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na hali ya rasilimali fedha itakaporuhusu tutawasiliananao na kushirikiananao kuhakikisha wanapata majukwaa kwa ajili kukamilisha uwanja wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika nimpongeze kwa juhudi kubwa ambazo amezifanya ikiwa ni pamoja na kuagiza nyasi bandia ambazo Serikali imezifutia kodi. Ninajua lengo lenu hasa ni kuhakikisha tunapata vipaji vingi kutoka Chunya kama ambavyo tumekuwa tukipata katika siku zilizopita na tunawaahidi tutashirikiana na ninyi kuhakikisha hilo linatekelezeka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; je, ni lini Serikali itaanza kujenga Uwanja wa Jamhuri wa Morogoro ambao unatumika kwenye michezo ya kitaifa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Jamhuri wa Morogoro ni miongoni mwa viwanja ambavyo tuko katika mpango wa kuvifanyia ukarabati mkubwa kwa ajili ya *AFCON 2027*. Siyo kwamba utachezewa rasmi mashindano yale, lakini ni viwanja ambavyo tunataka viwe tayari ili kama kuna timu inataka kuvitumia kwa ajili ya mazoezi na wenyewe utumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunaendelea kufanya mawasiliano na wamiliki wa uwanja huu kuona mpango ambao utatuwezesha kufanya ukarabati ule tukitumia fedha za umma, lakini Serikali isipate hasara na uwanja ule uweze kutumika na makundi yote ambayo tumepanga yanufaike na shughuli ambazo zinaweza kuendelea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Dkt. Ishengoma ya kwamba Uwanja wa Jamhuri wa Morogoro uko katika mipango yetu na utafanyiwa ukarabati hali kadhalika ikiwa ni miongoni mwa viwanja vitano ambavyo tunavifanyia ukarabati mkubwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza niipongeze Serikali kwa uwekezaji mkubwa unaofanywa kwenye viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninatamani kuuliza, ninyi kama *custodian* wa viwanja nchini mmeona taarifa za nchi jirani kama Kenya kwenye maandalizi ya viwanja vya *CHAN* kuna *red flag*. Sasa tulikuwa tunatamani kupata neno la matumaini sisi kama wanamichezo, maandalizi ya viwanja kwa ajili ya *CHAN* kwenye nchi yetu imefikia hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa *Senator* Festo Sanga. Sisi kama Tanzania maandalizi yetu ya viwanja kwa ajili ya *CHAN 2025* ambayo inatakiwa kuchezwa mwezi Agosti mwaka huu yanaendelea vizuri sana. Viwanja vyote viko katika hali nzuri kwa sababu viwanja ambavyo vitachezewa *CHAN* ni Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umekamilika ukarabati wake, lakini na Uwanja wa Amani – Zanzibar vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna viwanja vya mazoezi ambapo Dar es Salaam tuna viwanja vitatu; Kiwanja cha Shule ya Sheria, Kiwanja cha Gymkhana na Kiwanja cha Meja Jenerali Isamuhyo ambavyo vyote viko katika hatua nzuri. Hizi taarifa ambazo *CAF* wanazitoa ni taarifa za ukaguzi wa mara kwa mara na ziko kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maeneo ambayo wanataka yafanyiwe marekebisho yanafanyiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, ninaamini taarifa hii ambayo unaisema ya wenzetu Kenya imetoka kwa ajili ya kuwaelekeza nini wanatakiwa kufanya ili viwanja vyao viwe tayari kwa ajili ya *CHAN* ifikapo mwezi Agosti. Sisi kama Tanzania viwanja vyetu viko tayari hata wakitaka mashindano yachezwe mwezi ujao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo, tarehe 15 Mnyama yuko kwa Mkapa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Mnyama yuko kwa Mkapa, wakipambana na mahasimu wao Yanga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Mzava.

Na. 468

**Ujenzi Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Rufaa Shinyanga**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Shinyanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kiasi cha shilingi bilioni tatu kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Shinyanga. Kazi ya usanifu imefanyika na michoro imeandaliwa. Hatua iliyopo ni kutafuta mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi. Fedha za ujenzi wa jengo hilo itapelekwa kadri mkandarasi atakavyokuwa analeta madai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa umesema kwamba fedha zimeshatengwa na mkandarasi mnamtafuta; ni lini atapatikana mkandarasi ili aanze kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ili hospitali ikamilike ni lazima iwe na miundombinu yote. Hospitali ya Rufaa ya Shinyanga haina *maternity complex,* haina *pediatric ward,* haina *surgical ward,* haina *medical ward,* haina *laundry* na haina *mortuary*. Sasa ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba majengo hayo yanakamilika ili kweli ikidhi vigezo vya kuwa Hospitali ya Rufaa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimtoe Mheshimiwa Mbunge wasiwasi wa kwamba ni lini mkandarasi atakwenda *site?* Wala asiogope, mchakato ambao umetumika mpaka sasa hospitali hiyo mpya nzuri ambayo sawa ina upungufu wa baadhi ya majengo lakini imeanza ikafanyika ni mchakato huo huo na utawafikisha Wana-Shinyanga sehemu nzuri. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi ni mara moja katika kulingana na taratibu za manunuzi ambazo sisi wenyewe tumezipitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; majengo hayo mengine kwa kweli ni mchakato wewe unajua na ulikuwepo, mimi na Wabunge wenzako wakati Makamu wa Rais anakuja kuweka jiwe la msingi pale na kila wakati umekuwa ukiona majengo mbalimbali na hatua mbalimbali zikifikiwa. Kwa hiyo, tuwe wavumilivu kwa sababu unajua kuna mikoa mbalimbali ujenzi unaendelea, lakini kila maendeleo ni hatua. Kwa hiyo, tunaenda na hili jengo, lakini majengo mengine yote yataenda kufuatia kwa kadri pesa zinavyopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona, Kituo cha Afya cha Tarafa ya Matemanga hakina wodi ya mama na mtoto, wodi ya kina baba, na wodi ya watoto na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuwa kwenye ziara yake na kusimama katika kata ile kuzungumza na wananchi wa Matemanga aliahidi kujenga wodi hizo tatu.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi zile tatu na kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Waziri wetu Mheshimiwa Jenista Mhagama alitoa maelekezo mahsusi kwa zile ahadi za Rais sehemu zote kwenye afya ambako Rais ametoa ahadi na viongozi wengine wakuu patengwe hela na hela zimeshatengwa na mojawapo wa eneo lililotengewa hela ambao ni muda tu kazi ianze ni eneo lako hilo Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninapenda kumshukuru Waziri wa Afya, Mama yetu Jenista Mhagama kwa kufika *St. Francis Hospital,* (hospitali yetu ya rufaa) ambayo Serikali ina mashirikiano mazuri sana na Hospitali hiyo ya St. Francis.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Waziri pia na *Comrade CDF* kwa kutuletea Mkurugenzi mpya pale wa hospitali *Mr. Fusi,* anafanya kazi nzuri. Kwa kuwa Serikali ina mashirikiano na Hospitali ile ya Kanisa ina changamoto ya *CT-Scan* na jokofu; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka hiyo *CT-Scan* na jokofu ili wananchi waweze kupata huduma kwa bei nafuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Waziri alikwenda pale na ni kweli baada ya kurudi alituelekeza kwa kuzingatia makubaliano ya Serikali kuhusu mikataba ile ya Serikali ya ushirikiano na kanisa tuiangalie kwa pamoja ili tuweze kumpelekea ushauri ni namna gani tunaweza kushirikiana kwa pamoja ili tuweze kutatua hilo tatizo ambalo umelielekeza kwenye eneo hilo na ninakumbuka siyo mara ya kwanza wewe kulisema kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba atupe muda ili watalamu wachakate yale makubaliano tuone namna kwa pamoja tunaweza kufikia muafaka wa namna ya kutatua kwa pamoja hilo tatizo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Massare.

Na. 469

**Ujenzi wa Barabara ya Itigi – Noranga Kipande cha Mkiwa – Mlongoji**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza: -

Je, ni lini mkandarasi wa Barabara ya Itigi – Noranga ataanza kazi katika kipande cha Mkiwa – Mlongoji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Itigi eneo la Mlongoji hadi Mkiwa (kilometa 31.57) umesainiwa na kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za kulipa malipo ya awali ili Mkandarasi aanze kazi za ujenzi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu ulisainiwa mwaka 2023, leo ni miaka miwili na zaidi mkandarasi yuko *site* hajalipwa hayo malipo ya awali; je, ni lini watamlipa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande anachojenga sasa mkandarasi huyu *CHICCO* cha Mlongoji kwenda Noranga kilometa 25 nacho kimesimama. Je, ni lini Serikali itamlipa huyu mkandarasi *certificate* anazodai ili aweze kuendelea na kumalizia kipande hiki ambacho kimebaki kidogo tu ili wananchi wa Itigi na sisi tufaidi matunda ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupita katika barabara ya lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi alivyokuwa amesaini kazi aliyokuwa anafanya ni kufanya maandalizi ya awali. Sisi kama Serikali tunaendelea kufanya maandalizi ya kumlipa malipo ya awali ili sasa kazi ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuhusu swali lake la pili kwamba kipande cha Noranga kwenda Mlongoji tulishapokea hati za madai kwa maana ya kazi aliyofanya. Tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yuko asilimia zaidi ya 70 na tutahakikisha kwamba anakamilisha baada ya kumlipa fedha ambazo anaidai Serikali kwa kazi ambayo tayari ameifanya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; yupo mgeni wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ndugu Emmanuel Nyavike, mdau wa sekta ya ardhi na Mkurugenzi wa *Hello African Consultants* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, wapiga kura wake kutoka Chaani, Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, timu ya Tamthilia ya Toboa Tobo kutoka Jijini Dar es Salaam na Wilaya ya Nachingwea, Mkoani Lindi. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 50 wa Idara ya Saikolojia kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wanachama 42 wa Umoja wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Tawi la Chuo cha Mifugo na Uvuvi *(LITA)* Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wanachama 22 na Taasisi ya Wanautalii ndani na nje ya Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho tarehe 31 Mei, 2025 kuanzia saa 3.00 asubuhi wanaalikwa kuhudhuria Sherehe za kutoa Tuzo kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mfike kwa muda uliotangazwa kuheshimisha *protocol* ya mamlaka ambayo inayokuja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.27 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 2 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*